JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BENKI KUU YA TANZANIA

**06 Agosti 2026**

## TAARIFA KWA UMMA

## MAREKEBISHO YA KANUNI ZA FEDHA ZA KIGENI ZA MWAKA 2026

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha umma kuwa Kanuni za Fedha za Kigeni (Marekebisho) za Mwaka 2026 zimetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura ya 271, kupitia Tangazo la Serikali Na. 206 la mwaka 2026, lililochapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 17 Julai 2026.

Pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zinaruhusu wawekezaji wote wasio wakazi kuwekeza katika dhamana za Serikali za muda mfupi na muda mrefu zinazotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla ya marekebisho haya, ushiriki katika soko la dhamana za Serikali uliruhusiwa kwa wakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, na Watanzania waishio nje ya nchi pekee.

Hatua hii inalenga kupanua wigo wa ushiriki katika soko la dhamana za Serikali na ni sehemu ya jitihada za Benki Kuu za kuendeleza masoko ya fedha nchini na kuitangaza Tanzania kama kitovu chenye fursa za uwekezaji. Kanuni za Fedha za Kigeni (Marekebisho) za Mwaka 2026 zinapatikana katika tovuti ya Benki Kuu www.bot.go.tz

Hivyo, wawekezaji wasio wakazi wanaweza kuwekeza kupitia mawakala wa uwekezaji katika dhamana za serikali, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Fedha za Kigeni (Marekebisho) za Mwaka 2026, pamoja na sheria nyingine zinazohusika na taratibu za kiutendaji zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na mawakala wa uwekezaji katika dhamana za serikali au Benki Kuu ya Tanzania.

**Emmanuel M. Tutuba**
**GAVANA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: governoroffice@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501